Afronomicslaw

# HATIFUNGANI YA KIJANI YA MIUNDOMBINU YA MAJI YA MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA TANGA (TANGA UWASA)

Ufadhili Bunifu au Utegemezi wa Ufadhili wa Kigeni?

## Utangulizi

Barani Afrika, serikali ndogo (NCGs) (majimbo madogo, mikoa, miji, manispaa, serikali za mitaa, n.k.) zinakabiliwa na maongezeko ya athari za mabadiliko ya tabianchi. Makabiliano haya yamepelekea mabadiliko kwenye zana za ufadhili wa mabadiliko ya tabianchi, ili kukidhi upungufu wa ufadhili wa miradi ya upunguzaji na marekebisho ya ndani ya nchi. Mfano mmoja ni Hatifungani ya Kijani ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tanga (Tanga UWASA) nchini Tanzania-zana inayoibua maswali muhimu kuhusiana na wajibu wa madeni, kuweka kipaumbele miradi iliyo na faida kuliko mahitaji ya jamii, pamoja na hatari ya kufadhili huduma muhimu za umma.

Katika utafiti wao wa 2024, Ohiocheoya Omiunu pamoja na Ifeanyichukwu Azuka Aniyie walichunguza kama hatifungani hizi za Tanga UWASA zinawakilisha uhamasishaji wa kweli wa mtaji wa ndani au zinaimarisha utegemezi wa kifedha za kigeni. Watafiti hawa wanahoji ya kwamba hatifungani ya Tanga UWASA ni mfano wa ahadi na mitego ya kwenye ubunifu wa ufadhili wa miradi ya mabadiliko ya tabianchi barani Afrika, inayoficha matatizo yanayokabili serikali ndogo za Kiafrika (SNGs) wanapopitia usanifu wa kifedha wa kimataifa ambao unauwezo wa kuhudumia maslahi ya nje zaidi kuliko mahitaji ya maendeleo ya jamii.


> *Kwa upande wa Tanga, utaratibu wa hatifungani ya kijani unaweza kutoa suluhisho la kufadhili miundombinu ya maji- kwa muda mfupi, lakini kuna hatari ya mfumo huo kuweka kipaumbele kwenye kumrejeshea mwekezaji badala ya uendelevu wa muda mrefu, ambao utaongeza mzigo wa madeni ya Tanzania na kuweka uwezekano wa kudhoofisha utulivu wa kijamii na kiuchumi wa jumuiya hizo ambazo zilikusudiwa kuhudumiwa na mradi.*

## Hatifungani ya Kijani ni nini?

Kama hatifungani za kawaida, hatifungani za kijani ni mkopo unaotolewa na wawekezaji tofauti kwa wakati mmoja. Mkopo huo anapewa mtoaji wa hatifungani hizo ambaye ameazimia kulipa uwekezaji huo pindi utakapofikia ukomo, pamoja na kulipa riba thabiti au riba ya dhamani wakati wa umiliki au ukomo wa hatifungani hizo au kwa tarehe maalum ya ukomo wa uwekezaji huo. Sifa kuu ya hatifungani za kijani ni kwamba zinapanua wigo wa wawekezaji kwa mtoaji na huweka sifa za kimazingira zinazofanya watoaji kuwavutia wawekezaji wanaoweka kipaumbele kwenye mambo ya kimazingira, kijamii na utawala.

Kwenye muktadha wa Kiafrika, hatifungani za kijani zinaweza kuhusishwa na uwezo wake wa kufungua fursa kubwa za kiuchumi, kuepuka hasara kubwa za kiuchumi na kupunguza matokeo mabaya ya kijamii na kimaendeleo. Ingawa hatifungani za kijani zinavumbua njia zinazoweza kusukuma ukuaji wa uchumi na kuchochea ukuaji wa kodi, ni muhimu kukabiliana na utoaji wake kwa tahadhari. Kama zana za madeni, huweka majukumu ya ulipaji ambayo, yaiposimamiwa vyema, yanaweza kubatilisha faida zake za kiuchumi na kuweka mzigo mkubwa wa kifedha kwa mtoaji husika.





## Hatifungani ya Kijani ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tanga (Tanga UWASA) ni nini?

Hatifungani ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tanga (UWASA) ni hatifungani ya kijani ya kwanza kimataifa, Afrika Mashariki.[1] Imetolewa mwaka 2024, ni mfano wa kipekee unaohamasisha mapato ya serikali ndogo (SNG) kupitia soko la mitaji. Mradi huu ni matokeo ya ahadi ya kimazingira na kijamii ya Tanga UWASA pia unalenga kutatua changamoto kubwa za maji na usafi wa mazingira zinazoukabili mkoa wa Tanga nchini Tanzania, unaohusisha Jiji la Tanga na miji ya Muheza na Pangani.

Hatifungani ya Kijani ya Tanga UWASA inabeba kiwango cha riba thabiti 13.50% kwa mwaka, inayolipwa kwa malimbikizo kila mwaka, huku kiasi cha uwekezaji kikiweza kukombolewa kulingana tu na ukomo wa uwekezaji mwaka 2034. Malipo haya ya kutabirika na ya mara kwa mara yanafaulisha hatifungani ya Tanga UWASA kuwa hatifungani ya kikapu.[2] Hatifungani hii imeorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) na hivi karibuni iliorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Luxembourg (LuxSE).

## Ukweli Kuhusu Hatifungani ya Tanga UWASA

- Hatifungani ya kijani ya mapato ya miundombinu ya maji, ya miaka kumi, yenye thamani ya shilingi bilioni 53.12 (Dola za Marekani milioni 21).
- Imejengwa juu ya mkakati mbadala wa kufadhili miradi Tanzania- uliobuniwa ili kusaidia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP-III) unaolenga kukusanya rasilimali za ndani ili kufadhili miradi ya maendeleo ya kimiundombinu na utumishi wa umma.
- Kihistoria, ni hatifungani ya kijani ya maji, ya kipekee kimataifa na katika historia ya Tanzania na Afrika

## Udhaifu wa Mabadiliko ya Tabianchi kwenye NCG za Kiafrika

Udhaifu wa vituo vya mjini barani Afrika kwenye athari za mabadiliko ya tabianchi ni pamoja na kupanda kwa kina cha bahari, matukio ya hali ya hewa ya mara kwa mara na makali, na matatizo ya miundombinu ya umma inayoelemewa, pamoja na huduma zinazotishia maisha na ustawi wa mamilioni ya wakazi.[3]

Hata hivyo, mara nyingi watendaji kwenye jamii hukosa uelewa mpana wa mazingira ya ufadhili wa miradi ya mabadiliko ya tabianchi pamoja na uwezo wa kukidhi mahitaji magumu na mahitaji mengine yasiyowekwa wazi, yanayohusiana na mifumo mingi ya ufadhili, na uwezo wa kutambua na kutengeneza miradi inayoendana na viwango vya soko pamoja na mahitaji ya wawekezaji kwenye taasisi kubwa.[4] Hii inaendeleza mpaka kwenye uundaji wa vigezo dhabiti vya kustahiki au malengo kabambe ya uendelevu yanayowiana na matarajio ya kimazingira, kijamii na utawala (ESG) ya wawekezaji wa kimataifa huku mradi ukibaki kuwa wenye faida.[5] Kwa hiyo, kuna msisitizo unaokua dhidi ya uvumbuzi wa bidhaa za kifedha zinazolengwa kukidhi mahitaji ya kipekee ya NCG za Kiafrika.[6]

1. See UNCDF, Tanga UWASA Issues Historic Water Infrastructure Green Bond Valued at TZS 53.12 Billion, News (Feb. 22, 2024), https://www.uncdf.org/article/8664/tanga-uwasa-issues-historic-water-infrastructure-green-bond-valued-at-tzs-5312-billion; see also Tanga UWASA, Tanga Water Green Bond Framework, Republic of Tanzania, Ministry of Water (Sept. 2023), https://www.tangauwasa.go.tz/green_bond/Tanga%20UWASA%20Bond%20-%20Green%20Bond%20Framework.pdf; Republic of Tanzania, Ministry of Finance and Planning, The Third National Five Year Development Plan 2021/22 – 2025/29 (Nov. 2, 2021), https://www.mof.go.tz/uploads/documents/en-1636177646-The%20Third%20National%20Five%20Years%20Development%20Plan%20202126%20Final.pdf.
2. O. Blanchard, A. Amighini & F. Giavazzi, Macroeconomics: A European Perspective (2017).
3. David Dodman et al., Cities, Settlements and Key Infrastructure, inClimate Change 2022 - Impacts, Adaptation And Vulnerability: Working Group II Contribution To The Sixth Assessment Report Of The Intergovernmental Panel On Climate change 907, 921 (Hans-Otto Pörtner et al. eds., 2022).
4. See Jessica Omukuti et al., The Green Climate Fund and Its Shortcomings in Local Delivery of Adaptation Finance, 22 Climate Pol'y 1225, 1225–40 (2022), and Geoffrey Adonu, Towards Closing Africa's Climate Financing Gap: Scaling African Governments' Access to the Sustainable Bond Market, in Transforming Climate Finance in an Era of Sovereign Debt Distress 141, 153 (James Thuo Gathii, Adebayo Majekolagbe & Nona Tamale eds., 2023).
5. Adonu, supra note 4, at 154.
6. For a comprehensive overview of the origins and evolution of climate finance mechanisms at the local and municipal levels in Africa, see Climate Bonds Initiative, Data, https://www.climatebonds.net/market/data/#issuer-type-charts (last visited Dec. 22, 2024).

# Matokeo ya Utafiti

Uchambuzi wa utafiti ulibaini wasiwasi unaohusiana na utoaji wa hatifungani za Tanga UWASA, kama ifuatavyo:

**Athari kwa Sekta Binafsi:**
Utoaji wa Hatifungani ya Kijani ya Tanga UWASA kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam una uwezo wa kupunguza upatikanaji wa mitaji ya uwekezaji kwa sekta binafsi ndani ya nchi au kuongeza gharama yake (riba) pindi serikali inaposhindana na sekta binafsi kwa ajili ya mtaji mdogo unaopatikana katika soko la fedha la Tanzania, jambo ambalo lina sifa ya ukwai mdogo na kina.[7]

**Kutawala kwa Wawekezaji wa Kigeni:**
Uwezekano wa kutawaliwa na wawekezaji wa kigeni waliojisajili kwenye hatifungani una athari kadhaa zinazoenea katika nyanja za kiuchumi, kisiasa na kimkakati. Wageni wanaomiliki hatifungani wanaweza kuleta ushawishi mkubwa, nchini Tanzania, juu ya miundombinu ya kimkakati, na kuruhusu taasisi ya kigeni kuwa na udhibiti usio wa moja kwa moja juu ya utumishi muhimu wa umma, hasa pindi Tanga itakapokabiliwa na matatizo ya kiuchumi na kushindwa kulipa malipo yanayodaiwa kwenye hatifungani hiyo.

**Athari ya kifedha na madeni yasiyotarajiwa:**
Utoaji wa dhamana unaleta hatari ya kifedha na madeni yasiyotarajiwa kwa Tanzania.[8] Kwa sababu ya muundo na chanzo chake, hatifungani ya Tanga inaonekana kuwa deni ambalo lisingeingizwa kwenye mchakato wa usimamizi wa deni kuu la Tanzania. Kwa Tanzania, hii inaongeza hatari ya madeni yasiyotarajiwa kuongezeka na kutoorodheshwa.

**Madhara kwenye wasifu wa Deni Kuu:**
Hatifungani ikishatolewa inaongeza deni kuu la Tanzania, kwa kuongeza uwiano kati ya deni na Pato la Taifa na uwiano kati ya ufadhili wa hatifungani na Pato la Taifa, ambayo wakala wa viwango vya mikopo wakiwa kama 'walinda mlango' kwenye soko la mitaji na wawekezaji/wadai binafsi huzingatia wakati wa kuendesha maelezo ya deni kuu Tanzania katika siku za usoni.[9] Ongezeko la deni la Tanzania kunaweza kuathiri viwango vya nchi.

**Gharama za Makubaliano Zilizojificha:**
Utoaji wa hatifungani ya Tanga UWASA unahusisha gharama kubwa za makubaliano, zilizojificha, ambazo ni pamoja na upembuzi yakinifu, ushauri wa kisheria, uthibitishaji, ada za uorodheshwaji, na mahitaji yanayoendelea ya kuripoti yanayoidhinishwa na viwango endelevu vya kimataifa. Zaidi ya hayo, kuna gharama za ziada za kutathmini ustahili wa mikopo na uthibitishaji wa wahusika wengine wa kimazingira, kijamii, na utawala (ESG) ambazo zinaweza kuanzia Dola za Marekani 10,000 hadi Dola za Marekani 100,000, zinazolipwa ili kuvutia wawekezaji wa kitaasisi katika masoko ya kimataifa kama vile Luxemburg. Gharama hizi za makubaliano zinahatarisha kupunguza mapato halisi ya utoaji.

**Kutotekelezeka kwa Vigezo vya Kijani:**
Memoranda ya taarifa ya Hatifungani ya Kijani ya Tanga UWASA inaelezea ya kwamba mapato ya hatifungani hizo yatatumika kufadhili upya, kwa ujumla au sehemu ya miradi mipya au iliyopo, inayostahiki (usimamizi endelevu wa majisafi na maji machafu, nishati mbadala, ufanisi wa nishati, na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi).[10]

### Madhara ya Hatifungani ya Tanga UWASA kwa Tanzania

- Kuhamisha wateja binafsi wa bidhaa za soko la mitaji na mdororo wa uchumi.
- Kutawala kwa wawekezaji wa kigeni.
- Kuunda hatari ya kifedha na madeni yasiyotarajiwa kwa Tanzania.
- Kuzorota kwa wasifu wa deni kuu.
- Gharama za makubaliano zilizojificha.
- Viwango vya kijani kutotekelezwa kisheria
- Kuhalalisha biashara zenye mashaka.
- Mtengamano katika umma.
- Kuongezeka kwa gharama.
- Ukosefu wa faida.

7. Id.
8. H. Polackova, Contingent Government Liabilities: A Hidden Fiscal Risk, 36 Fin. & Dev. 46, 46–49 (1999).
9. D. Cash, Sovereign Debt Sustainability: Multilateral Debt Treatment and the Credit Rating Impasse (2023).
10. See UNCDF, Tanga UWASA Issues Historic Water Infrastructure Green Bond Valued at TZS 53.12 Billion, News (Feb. 22, 2024), at 39, https://www.uncdf.org/article/8664/tanga-uwasa-issues-historic-water-infrastructure-green-bond-valued-at-tzs-5312-billion.

Hata hivyo, hakuna maagano madhubuti au sahihi, yanayoweza kutekelezeka kisheria, yanayomlazimu mtoaji kutii viwango ambavyo hatifungani ya 'ukijani' imewekwa, na athari ya hii ni kuunda hisia za matumaini juu ya 'ukijani' wa hatifungani hizi. Hii inazua wasiwasi juu ya upotofu wa miradi ya kijani, kwa sababu hatifungani hizi zinakuwa hazina utofauti na hatifungani za kawaida.

- **Uthibitisho wa Biashara yenye Mashaka:**
  Kwa makadirio ya ongezeko la upatikanaji wa maji kutoka 96% hadi 100% katika Jiji la Tanga, kwa upande wa kibiashara na uhalali wa kiuchumi wa mradi uliofadhiliwa na hatifungani hii unatia shaka.

- **Mtengamano katika Umma:**
  Kwa suala la hatifungani ya Tanga UWASA, Memoranda ya Taarifa ya 2024 haina ushahidi ya kwamba kulikuwa na mashauriano ya moja kwa moja na jumuiya za mitaa kuhusiana na malengo ya mradi, athari zinazotarajiwa na hatua za kumudu gharama hizo. Hii inazua wasiwasi ya mtengamano kati ya vipaumbele vyao na malengo ya mradi dhidi ya mahitaji halisi ya wakazi wa eneo hilo. Marejeleo ya ushirikshwaji wa wadau umekadiriwa kwa watendaji wa kitaasisi pekee, wakiwemo watendaji wa soko, wadhibiti, wanateknolojia, na warasimu. Uwazi na ushirikishwaji bora wa wadau ni muhimu kwenye kuhakikisha kwamba miradi inayofadhiliwa na hatifungani za kijani, kama Hatifungani ya Kijani ya Tanga UWASA, inashughulikia mahitaji ya jumuiya zisizohudumiwa badala ya kutanguliza maslahi ya wawekezaji pekee.

- **Hatari ya kuongezeka kwa gharama:**
  Miradi mikubwa ya kimiundombinu inakabiliwa na ongezeko la gharama. Kwa upande wa mradi wa hatifungani wa Tanga UWASA, huu ni ukweli unaowezekana, kwani inawezekana kuwepo na makadirio ya gharama yasiyo sahihi. Mabadiliko ya kiwango cha ubadilishaji fedha, mfumuko wa bei, na uorodheshaji wa kwenye LuxSE hivi karibuni ni uhalisia mwingine unaoweza kuleta ongezeko la gharama.

- **Ukosefu wa Faida:**
  Ili hatifungani ionekane kuwa yenye faida, inapaswa kuwa na uwezo wa kuzalisha mtiririko wa pesa unaolingana, aidha kutokana na mapato yanayozalishwa au kuokoa gharama kutokana na ufanisi wa nishati, hasa hatifungani zilizoundwa kufadhili miradi ya ESG. Kulingana na mwanasheria wa kimataifa Geoffrey Adonu, huu ni upungufu mkubwa unaohusishwa na hatifungani zinazotolewa na serikali za Kiafrika.[11] Uwezekano mdogo wa kuanzishwa kwa soko mbadala la uwekezaji ambalo lingewapa wawekezaji fursa ya kuuza mali zao kwa urahisi, au kwa bei ambayo itatoa mavuno kulinganishwa na uwekezaji sawa na njia mbadala iliyotengenezwa, ni msingi wa kutilia shaka faida ya Hatifungani ya Kijani ya Tanga UWASA.

> *Hakuna maagano madhubuti au sahihi, yanayoweza kutekelezeka kisheria, yanayomlazimu mtoaji kutii viwango ambavyo hatifungani ya 'ukijani' imewekwa, na athari ya hii ni kuunda hisia za matumaini juu ya 'ukijani' wa hatifungani hizi.*

> *Uwazi na ushirikishwaji bora wa wadau ni muhimu kwenye kuhakikisha kwamba miradi inayofadhiliwa na hatifungani za kijani, kama Hatifungani ya Kijani ya Tanga UWASA, inashughulikia mahitaji ya jumuiya zisizohudumiwa badala ya kutanguliza maslahi ya wawekezaji pekee.*



11. Adonu, supra note 4, at 154.

# Mambo Muhimu ya Uchambuzi wa Hatifungani ya Kijani ya Tanga UWASA

- Utegemezi wa hatifungani za kijani kama aina ya uhamasishaji wa rasilimali zinazofadhiliwa na madeni huleta madeni ya muda mrefu ambayo yanaweza kuongeza wasifu wa deni la Tanzania, haswa ikiwa makadirio ya mapato yatapungua au gharama za makubaliano zikapanda.

- Ingawa Hatifungani ya Kijani ya Tanga UWASA inalingana na mienendo ya kawaida inayotarajiwa kwenye hatifungani ya aina hii, uwezekano wa gharama kubwa za miamala, ushawishi wa matarajio ya wawekezaji wa kimataifa, na hatari ya kutanguliza faida juu ya mahitaji ya umma yanaangazia maeneo muhimu ya kuchunguzwa.

- Ingawa IMF bado inaona kwamba, kifedha, Tanzania bado ina uwezo wa kuongezea deni, mabadiliko haya ya kuelekea katika uhamasishaji wa rasilimali za ndani kwa mfumo wa Hatifungani ya Kijani ya Tanga UWASA lazima yafuatiliwe kwa karibu ili kuhakikisha kwamba hayawi mabomu yanayoweza kulipuka muda wowote.

- Kwa upande wa Tanga, utaratibu wa hatifungani ya kijani unaweza kutoa suluhu ya muda mfupi ya kufadhili miundombinu ya maji, lakini inahatarisha kuanzisha mfumo unaoweka kipaumbele kwenye mapato ya wawekezaji badala ya uendelevu wa muda mrefu, na hivyo kuongeza mzigo wa deni la Tanzania na kuwezekana kudhoofisha utulivu wa kijamii na kiuchumi wa jumuiya ambazo mradi unakusudiwa kuhudumia.

- Wakati hatifungani ya Tanga UWASA inatoa fursa muhimu kwa serikali ndogo (SNG) kutumia mfumo na muundo wa kitaifa kuongeza mtaji mkubwa, uorodheshaji wa hatifungani hivi karibuni kwenye LuxSE uliibua maswali kuuliza kama hii inafanya uhamasishaji wa rasilimali za ndani au za kimataifa. Hitimisho ni kwamba tukio la karibuni linachanganya zaidi uainishaji wa hatifungani hii kwa kuchukua usajili hadi nje ya mipaka ya Tanzania (taasisi za ndani au raia).

*INGAWA IMF BADO INAONA KWAMBA, KIFEDHA, TANZANIA BADO INAYO UWEZO WA KUONGEZA DENI ZAIDI, MABADILIKO HAYA YA KUELEKEA KATIKA UHAMASISHAJI WA RASILIMALI ZA NDANI KWA MFUMO WA HATIFUNGANI YA KIJANI YA TANGA LAZIMA YAFUATILIWE KWA KARIBU ILI KUHAKIKISHA KWAMBA HAYAWI MABOMU YANAYOWEZA KULIPUKA KWA WAKATI WOWOTE.*

# Kusawazisha Uvumbuzi na Busara:

## Mapendekezo kwa Serikali za Mitaa Zinazohesabia Hatifungani za Kijani

Hatifungani za kijani zinatoa njia inayoweza kuchochea uhamasishaji wa rasilimali za ndani kwa muda mrefu- kwa kuendesha upanuzi wa uchumi na kuchochea ukuaji unaotozwa kodi. Hatifungani ya Kijani ya Tanga UWASA inawakilisha mpango wa kihistoria wa kufadhili miundombinu endelevu katika ngazi ya nchi ndogo barani Afrika. Hata hivyo, uchanganuzi wa utafiti huu unadhihirisha kwamba mbinu hii haikosi mashaka makubwa ambayo yanapaswa kushughulikiwa katika muktadha wa utoaji wa hatifungani ya Tanga UWASA na zana zozote za baadaye za aina moja ambazo zitatakiwa kuchipuka katika bara zima la Afrika. Waandishi wa utafiti huu wanapendekeza hasa miradi inayosawazisha uvumbuzi wa kifedha wa hatifungani za kijani kwa wenyeji pamoja na mbinu ya busara na ya tahadhari ili kuepusha athari mbaya za kiuchumi, kutawala kwa wawekezaji wa kigeni, upotofu wa miradi ya kijani, na mtengamano katika umma.  Mbali na ufuatiliaji wa karibu wa utoaji wa hatifungani, waandishi wanapendekeza yafuatayo:

- Kupitisha ulinzi wa hatifungani za kijani zinazolenga huduma muhimu ili kuzuia uhamisho wa kiuchumi, pamoja na kutoa masharti ya ufikaji wa bei nafuu na mbinu za kufuatilia matokeo ya mradi wa kijamii na kiuchumi, baada ya muda.

- Kuhakikisha ushiriki wa mapema na wa maana kwa jamii zilizotengwa kwenye mchakato wa kutunga sera.[12]

- Kujumuisha mfumo wa wazi wa watumiaji, kama vile kutathmini uwezo wa umma kumudu ongezeko linalowezekana la ushuru wa huduma za umma, ambalo linaweza kuoanisha mradi zaidi na malengo yanayozingatia usawa, kupunguza hatari ya kwamba wakazi wa kipato cha chini wangebeba mizigo ya kifedha.

- Kutoa taarifa za uwazi za kimazingira, kijamii, na utawala (ESG) na kutoa taarifa za mara kwa mara kwa umma kuhusu mgao na athari za hatifungani. Kutumia mbinu hizi bora kunaweza kuboresha uaminifu na athari za kijamii kwenye umma, ikisaidia kuhakikisha kwamba maslahi ya wawekezaji wa kimataifa hayafuniki mahitaji ya kijamii na kiuchumi ya wakazi wa eneo hilo.

*Kupitisha ulinzi wa hatifungani za kijani zinazolenga huduma muhimu ili kuzuia uhamisho wa kiuchumi, pamoja na kutoa masharti ya ufikaji wa bei nafuu na mbinu za kufuatilia matokeo ya mradi wa kijamii na*



12. US-EPA, Municipal Bonds and Green Bonds (Apr. 11, 2024), https://www.epa.gov/statelocalenergy/municipal-bonds-and-green-bonds (last visited Nov. 3, 2024).